



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU**



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.NDC/S.20/12/VOL.III/48

Tarehe 14 Agosti, 2023

### TANGAZO LA NAFASIZA KAZI

Kwa mujibu wa Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb.Na.FA.97/362/01"B"/85 cha tarehe 26 Juni 2023 kutoka kwa katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III.

#### 1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - (NAFASI 03)

##### 1.1 SIFA:

Mwombajii awe amefaulu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti 'NTA Level 5' katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Usimamizi wa Serikali za Mitaa, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamiziwa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### 1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III:

- 1) Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Kijiji,
- 2) Kusimamia masuala ya usalama, kudumisha amani na utulivu katika kijiji;
- 3) Kuandaa, kupitia na kutekeleza mipango na Bajeti za Maendeleo ya Kijiji;
- 4) Kusimamia, kukusanwa na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Serikali ya Kijiji;
- 5) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji;
- 6) Kutoa huduma za ukatibu kwa vikao vya kamati na Halmashauri ya Kijiji;
- 7) Kutafsiri na kutekeleza sera, sheria na taratibu za kisekta katika ngazi ya Kijiji;
- 8) Kufuatilia utekelezaji wa mipango na bajeti ya Kijiji;
- 9) Kuandaa, kupitia na kutekeleza Sheria Ndogo za Kijiji;

- 10)Kuratibu na kushughulikia usimamizi wa maafa;
- 11)Kushughulikia malalamiko ya wananchi;
- 12)Kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika Kijiji; na
- 13)Atatekeleza majukumu mengine kadiri atakavyopangiwa na Mtendaji wa Kata.

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA:

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kina ngazi ya Mshahara ya TGS B

### 1.4 MASHARTI YA JUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kwenye anuani iliyotajwa hapo chini;
- Mwombaji aambatishe nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, wasifu (Curriculum Vitae) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha mbili (Passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Testimonials "provisional results", "statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLEEPS) **HAVITAKUBALIKA;**
- Nafasi ya kazi inayoombwa iandikwe kwenye kichwa cha habari cha barua, kutozingatia hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili;
- Wombaji waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), au Namba ya Kitambulisho kwa ambao bado hawajapatiwa vitambulisho;
- Waombaji watakaokidhi sifa ndio watakaoitwa kwenye usaili (interview);
- Barua za maombi zinaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, na kutumwa/kuwasilishwa kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo: -

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALIUASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU,  
S.L.P 246,  
**MASASI – NANYUMBU.**

NB: Uwasilishaji wa barua za maombi kwa njia ya mkono katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya hauruhusiwi na hazitapokelewa, na Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe **25 Agosti, 2023 saa 9:30 Alasiri.**



Rudrick B. Charles

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

